Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

# Waraka wa Kairo wa kueneza Amani

## Mapendekezo ya Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa Ishirini na saba

## Baraza Kuu la Mambo ya Kiisilamu

## Wizara ya Waqfu ya Misri

**Chini ya usimamizi wa Mhe. Raisi / Abdulfatah Al sisi raisi wa Jamhuri ya kiarabu ya Misri. Na uongozi wa Profesa Muhammad Mukhtar Juma, Waziri wa Waqfu na Kiongozi wa Baraza Kuu la Maswala ya Kiisilamu. Wasomi wa dini, wana siasa, wabunge, wachambuzi, na wataalamu kutoka mataifa mbali mbali ulimwenguni wamekusanyika katika Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa Ishirini na saba ulioandaliwa na Baraza Kuu la Maswala ya Kiisilamu ambao umefanyika katika mkoa wa Kairo siku ya Jumamosi na Jumapili 13-14 Jamad Alakhar 1437H. sawa na tarehe 11-12/3/2017 A.D. chini ya anuani "Nafasi ya kiongozi na watenegezaji maamuzi katika kueneza amani na kupambana na ugaidi na changamoto".**

**Na baada ya kufululiza kazi kwa siku mbili kwa kufanyika vikao saba vya kielimu walioshiriki walimaliza vikao vyao kwa kutoa "Waraka wa Kairo wa kueneza amani" ambao unabeba ujumbe wa amani kwa ulimwengu mzima. Na una lengo la kueneza utamaduni wa amani kimaneno na kimatendo chini ya programu na kufanya warsha (majukwaa ya kuelimisha) na sheria ili kufikia lengo na kufanikisha maisha mazuri ya pamoja kwa wanadamu, pamoja na kuzingatia mapendekezo yafuatayo:-**

**1- Umuhimu wa kubadilisha na kujibu tendo kwa matedo, na kueneza utamaduni wa amani kwa kupitia programu ya kuishi kiutu katika uhalisia kwa kiwango cha kitaifa na kwa kiwango cha ubinadamu na kimataifa.**

**2- Umuhimu wa kuzingatia ushirikiano wa kibinadamu na tafauti iliopo baina ya dini katika uhubiri wa dini, utamaduni,kitabia na kiutangazaji. Na kuweka sheria ambazo zitaharamisha ubaguzi kwa visingizio vya dini au rangi au ukabila.**

**3- Kufanya kazi kwa kupitia mashirika ya kimataifa katika kupinga ubaguzi kwa sababu za kidini au ukandamizaji wa dini bila ya kubagua.**

**4-Kuhakikisha kuwa ugaidi haufungamanishwi na dini ambazo ziko mbali sana na tendo hili, na kuweka wazi kuwa kufungamanisha ugaidi na dini ni dhuluma kubwa sana, na utaingiza ulimwengu katika matatizo ambayo hayatamalizika na wala kuondoka.**

**5-kufanya kazi katika kujenga misingi madhubuti ya usawa katika haki na wajibu katika ubinadamu na utaifa, na kupenda zaidi utaifa ambao ni milki ya raia wote, na kukuza hisia za ubinadamu na kuthibitisha misingi ya kuishi pamoja baina ya watu wote.**

**6-Ulazima wa kuamini utafauti na kuheshimu dini au rangi au utaifa, na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya masilahi ya taifa na wanadamu.**

**7-Ulazima wa wataalamu wa kidini kusahihisha ufahamu uliopotoshwa wa aya na hadithi ambazo magaidi huzitumia katika kuhalalisha**

**matendo yao maovu ya kigaidi na kufanya nao kongamano ili waweze kulete ufahamu ulio sahihi.**

**8-kutumia njia zote zilizopo za kukumbushia, kufundishia na za utangazaji: kama misikiti, mashule, vyuo vikuu, vituo vya vijana, majumba ya tamaduni, vyombo vya habari – runinga, redio, magazeti- ili kueneza utamaduni wa amani na kupambana dhidi ya fikira potofu na kuweka ufahamu sahihi kwa mambo yaliyopotoshwa pamoja na kuwepo ulazima wa kuchukua mafunzo ya lazima na endelevu ya kutaamali na vyombo hivyo.**

**9-Kuzidi kutumia mitandao ya kijamii na vyombo vya utangazaji vya kisasa kwa ajili ya kueneza utamaduni wa usamehevu na amani na kupambana na fikira potofu.**

**10-kujali nafasi ya mwanamke katika ufanyaji wa kazi na utamaduni na utangazaji na kielimu kutokana na nafasi yake kubwa na yenye athari ya wazi katika nyanja hizi na hasa katika nyanja za kukuza malezi ya kizazi juu ya tabia, maadili mema na uzalendo.**

**11-Ulazima wa kuwa na mawasiliano na viongozi wa mabunge kote duniani kwa ajili ya kuweka mipaka ya ufahamu wa ugaidi na kuweka pia sheria ya pamoja yenye kukemea ugaidi na fikira potofu pasi na kuangalia matendo hayo hutendwa na watu wa dini gani au utaifa gani au nchi gani. Na kutenda kwa pamoja katika kuharamisha matendo ya kuwapa hifadhi magaidi au kuwapa ruzuku kwa njia yoyote ile na inahitajika\inageuzika jambo hilo liwe kwa uhalisia na sio kwa baadhi tu.**

**12-Wito kwa bunge la Misri na mabunge mengine yote ulimwenguni kufanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya kuharamisha ugaidi wa mitandaoni kwa aina zake zote na kwa njia zake zote.**

**13-ulazima wa kuwepo na mawasiliano baina ya wasomi wa dini na watambuzi na wanasiasa na watangazaji, pia kuwepo na mawasiliano baina ya viongozi wa kidini tafauti kwa ngazi zote ili kuondosha kizuizi- kipingamizi- cha kinafsi katika kutendeana na watu tafauti. Kwani asiyejua kitu huwa ni adui wa kitu hicho, na njia yetu ni kuwa pamoja na sio kuwa mbalimbali, kuhurumiana na sio kuuana na kupigana, na kuthibitisha zaidi kuwa kutafautiana na hali ya kawaida ya ulimwengu, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: { Na kama Mola wako Angalipenda, bila shaka Angaliwafanya watu kuwa umati mmoja. Nao wataendelea kuhitilafiana* Isipokuwa yule ambaye Mola wako Amemrehemu; na kwa (rehema)hiyo Amewaumba.} (Hud; 118-119).**

**14-Ulazima wa kupambana na ugaidi na fikira potofu na kueneza utamaduni wa amani katika jadweli za mikutano ya kisiasa ili kuweza kusaidiana katika kuweka mikakati ya kimataifa ya kupambana na hali hiyo.**

**15-ulazima wa kubadilishana taarifa na matokeo ambayo viongozi wa kidini wameuanzisha na kuleta matunda yaliyotarajiwa katika kuwasilisha hutuba za kidini na utamaduni wa amani na usamehevu na kupinga hutuba zenye chuki na kutumia nguvu na kuweza kuchagua lililo bora. Na faida iliyopo ni kuweka mikakati ya ukweli katika**

**kupambana kwa njia na mipango ya mijadala katika warsha na programu za mafunzo tafauti.**

**16-Kuzidisha uwezo wa vyombo vya taifa kwa nchi zote zinazoamini kwa amani ili kuzidisha uwepo wa amani kwa kuwafanya wawe na uwezo wa kukabiliana na makundi yenye fikira potofu. Na hasa kwa kutumia vyombo vya kisasa pamoja na mikakati katika vyombo vya utangazaji kwa kuweka wazi kwa kueneza utamaduni wa amani na kukuza hisia za kitaifa na ubinadamu na kusahihisha ufahamu usio sahihi.**

**17-Ufasiri wa mapendekezo haya ya waraka utumwe katika bunge la Misri na kwa mabunge tafauti ulimwenguni, na kuutuma katika Wizara za Mambo ya nje na katika taasisi za kimataifa zinazohusika kwa ajili ya kueneza amani na kupambana na fikira potofu na ugaidi.**

**Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuwafikisha**
**na ndie aongozaye njia iliyo sahihi.**